



KATIBA YA KANISA LA

REDEEMED
ASSEMBLIES *of*
GOD TANZANIA

YA MWAKA 2024

Makao Makuu ya Kanisa
Kiwanja Na. 1, Kitalu C,
Kinyambwa Extension Area,
Simu: +255 (0) 743 774 888,
Barua Pepe: ragtanzania@gmail.com,
Sanduku la Posta: 2447 Dodoma.

DIBAJI

- Utangulizi Sisi **Redeemed Assemblies of God Tanzania (RAGT)**, kwa lengo la kuunda Umoja, Upendo, Amani, Haki, Usawa na Maongozi ya pamoja katika Kuhubiri Injili ya Yesu Kristo, tunatunga Katiba hii kwa ajili ya Kutuongoza katika Majukumu yetu ya kila siku.
- Uwepo Kutakuwepo Dhehebu la Kipentekoste ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lenye Jina la **Redeemed Assemblies of God Tanzania (RAGT)**, lililosajiliwa kisheria na Mamlaka ya Serikali Tarehe **23/06/1994**, kwa Cheti cha Usajili Na. SA. 8115, na litakaloendeshwa kwa Mujibu wa Katiba hii.
- Jina la Katiba Katiba hii itajulikana kama *“Katiba ya Kanisa la Redeemed Assemblies of God Tanzania ya Mwaka 2024”*.

YALIYOMO

TAFSIRI.....	vii
1. SURA YA KWANZA: TAARIFA ZA KANISA.....	1
2. SURA YA PILI: USHIRIKA NDANI YA RAGT.....	3
3. SURA YA TATU: MALENGO, IMANI NA MWONGOZO.....	7
4. SURA YA NNE: UONGOZI.....	11
5. SURA YA TANO: MIKUTANO NA VIKAO.....	27
6. SURA YA SITA: FEDHA NA MALI.....	35
7. SURA YA SABA: UCHAGUZI WA VIONGOZI.....	43
8. SURA YA NANE: UTATUZI WA MIGOGORO.....	53
9. SURA YA TISA: MABADILIKO YA KATIBA.....	55
10. SURA YA KUMI: BODI YA WADHAMINI.....	57
11. SURA YA KUMI NA MOJA: IDARA NA KURUGENZI	59

12. SURA YA KUMI NA MBILI: KUVUNJIKWA KWA
DHEHEBU..... 61
13. SURA YA KUMI NA TATU: MENGINEYO..... 63

TAFSIRI

Maana ya maneno yaliyotumika katika katiba hii, isipokuwa maelezo yakihitajika vinginevyo, yana maana ya;

Askofu Ni Mwenyekiti.

Huduma Ni Utumishi.

Kafara Ni Sadaka.

Kudhihirisha Ni kufunua/kuweka wazi.

Kuhuisha Ni kurejesha Uhai.

Kuokoka Ni kufanywa upya maisha ya mtu ndani ya Yesu Kristo (2 Kor 5:17).

Maono Ni udhihirisho juu ya mambo ya Mungu rohani.

Mauti Ni kifo cha roho (Mwanadamu kwenda motoni milele).

Mwito Ni agizo/mwaliko wa kuwaleta watu kwa Yesu Kristo.

Mwongozo Ni kanuni na taratibu mbalimbali za Uongozi na Utumishi wa Kanisa la RAGT.

RAGT	Ni kifupisho cha Jina la dhehebu la Redeemed Assemblies of God Tanzania.
Rohoni	Ni ndani ya mtu/kusikoonekana.
Uongozi	Ni kuwahudumia watu katika mahitaji yao ya Roho na Mwili.
Uongozi wa Pamoja	Ni uongozi wa Majadiliano na Makubaliano.
Uongozi wa Mungu	Ni uongozi wa Roho Mtakatifu katika nafsi tatu (Baba, Mwana na Roho Mtakatifu).
Uzima	Ni uhai wa milele.
Wokovu	Ni imani inayogeuza maisha ya mtu yawe na matumaini katika Kristo Yesu.
Kuwajibika	Ni kuwa na jukumu la kufanya kwa kuzingatia ngazi za Maongozi.
Kuwajibishwa	Ni kupewa jukumu la kufanya kwa kuzingatia ngazi za Maongozi, hususani kwa kosa lililotendwa na mtu/kiongozi.
Sekretarieti	Ni kikao cha Utendaji kazi wa shughuli za kila siku za RAGT.
CPCT	Ni kifupisho cha Baraza la Makanisa ya Kipentekoste Tanzania yaani THE COUNCIL OF PENTECOSTAL CHURCHES OF TANZANIA.

SURA YA KWANZA

TAARIFA ZA KANISA

Jina la
Dhehebu

1. Jina la Dhehebu ni Redeemed Assemblies of God Tanzania kwa kifupi RAGT, ikiwa na tafsiri ya *“Kusanyiko la Watu wa Mungu Waliokombolewa”*.

Mawasiliano
na Anwani

2. Simu ya Ofisi: +255 (0) 743 774 888,
Barua Pepe: ragtanzania@gmail.com,
Sanduku la Posta: 447 Dodoma.

Makao Makuu
ya Dhehebu

3. RAGT itakuwa na Ofisi Kuu na Ofisi ndogo

3.1 Ofisi Kuu ya RAGT itakuwa;
Kiwanja Na. 1, Kitalu C
Kinyambwa Extension Area,
DODOMA.

3.2 Ofisi ndogo za RAGT zitakuwa kwenye kila
Kanda Tanzania.

Nembo

4. Nembo rasmi ya RAGT iliyosajiliwa kwa Namba
TZ/S/2022/1056 ina alama zifuatazo;

4.1 Umbo la Duara lenye maandishi yanayosomeka REDEEMED ASSEMBLIES OF GOD TANZANIA.

4.2 Hua (Njiwa) ikiwa ni alama ya Roho Mtakatifu, pamoja na Miale ya Njano mdomoni mwake ikiwa ni Ishara ya Nguvu za Roho Mtakatifu.

4.3 Msalaba wenye rangi nyekundu ukiwakilisha damu ya Yesu Kristo iliyomwagika Msalabani kwa Ondoleo la dhambi za wanadamu.

4.4 Biblia chini ya Msalaba yenye rangi ya Ukijani katikati, ikiwa ni ishara ya Malisho mabichi kutoka kwenye Neno la Mungu lililo hai.

4.5 Neno R.A.G.T chini ya Nembo ikiwa ni kifupi cha Jina la dhehebu yaani REDEEMED ASSEMBLIES OF GOD TANZANIA.

Muonekano wa
Nembo



SURA YA PILI

USHIRIKA NDANI YA RAGT

Aina za Ushirika 5. Ndani ya RAGT tutakuwa na Ushirika wa aina mbili (2), ambao ni;

5.1 Mshirika

5.2 Mfuasi

Sifa za Mshirika 6. Ili mtu atambulike kuwa ni Mshirika wa RAGT atapaswa kuwa na sifa zifuatazo;

6.1 Awe ameokoka na kushuhudiwa kuwa ameokoka.

6.2 Awe amebatizwa ubatizo wa Maji mengi.

6.3 Awe ameabudu Kanisa la Mahali pamoja kwa kipindi kisichopungua miezi sita (6) mfululizo.

6.4 Ikiwa ameo/kuolewa, awe na ndoa ya mke/mme mmoja. Ndoa hiyo iwe ya watu wawili wa jinsia mbili tofauti.

6.5 Awe na ndoa ya Kikristo, yaani ndoa iliyofungwa Kanisani.

Wajibu wa
Mshirika

7. Wajibu wa Mshirika utakuwa ni;

7.1 Kumuheshimu Mchungaji na Viongozi wengine wa Kanisa.

7.2 Kuwaleta watu wengine kwa Yesu Kristo.

7.3 Kuishi maisha matakatifu yenye ushuhuda mzuri.

7.4 Kuhudhuria ibada za Kanisani kwa uaminifu.

7.5 Kutoa sadaka na fungu la kumi kwa uaminifu.

7.6 Kuchangia maendeleo ya Kanisa.

Haki za
Mshirika

8. Kila Mshirika ana haki ya;

8.1 Kupokelewa rasmi kanisani.

8.2 Kubatizwa na kupokea cheti cha Ubatizo.

8.3 Kufungishwa Ndoa kwa mujibu wa Sheria za Kanisa na Nchi.

8.4 Kushiriki Meza ya Bwana.

8.5 Kuchagua au Kuchaguliwa kuwa kiongozi.

8.6 Kuhudumiwa kiroho na kimwili, yaani kufundishwa Neno la Mungu na Misaada mbalimbali.

8.7 Kuhudumu kwa Neno na maeneo mengine ikiwa Mchungaji wake ataona ana uwezo huo.

8.8 Kuzikwa Kikristo.

8.9 Kushiriki shughuli mbalimbali za kikanisa.

8.10 Watoto wa Mshirika wana haki ya Kubarikiwa na kupewa Cheti cha Ubarikio.

8.11 Kujua Katiba na Miongozo mbalimbali ya RAGT.

Kukoma
Ushirika

9. Mtu yeyote atakoma Ushirika ndani ya RAGT endapo;

9.1 Atapoteza Sifa za Ushirika wa RAGT kama zilivyoainishwa kwenye Sura hii, Ibara ya Pili (2), na hivyo atakuwa amepoteza Haki zake zote kama Mshirika kwa mujibu wa Katiba hii.

9.2 Ametenda dhambi/Kosa au kukiuka Katiba hii na asipokuwa tayari kutubu/kugeuka/kubadilika/kufanya marekebisho.

Dokezo *Mtu akihama kutoka eneo moja kwenda lingine kwa taarifa, na akaendelea kuwa na Sifa za Mshirika wa RAGT, mtu huyo bado ataendelea kutambulika kama Mshirika wa RAGT.*

Mfuasi 10. Ni mtu yeyote aliyeamini/aliyeokoka katika moja ya Huduma za RAGT au kujiunga na Kanisa lolote la RAGT na ambaye bado hajatimiza Sifa za kuwa Mshirika zilizoainishwa kwenye Sura hii, Ibara ya Pili (2).

SURA YA TATU

MALENGO, IMANI NA MWONGOZO

Malengo ya
Dhehebu

11. Kutokana na Imani yake kwa mujibu wa Katiba hii, RAGT ina majukumu yafuatayo;

11.1 Kuhubiri Injili ya Yesu Kristo kwa watu wa Imani zote, ndani na nje ya Tanzania.

11.2 Kuanzisha/Kuimarisha makanisa mahali ambapo pataendelea kutoa habari njema yenye kuhuisha watu.

11.3 Kuhakikisha kwamba makanisa yanasimama katika Neno la Mungu (Biblia Takatifu) kwa kutoa mafundisho.

11.4 Kutoa huduma za Kiroho, Kiakili na Kimwili zinazohusu uzima na ustawi kama Elimu, Afya, Kilimo, Chakula, Lishe, Uvuvi, Michezo, pamoja na kutoa misaada kwa watu waishio katika mazingira magumu ikiwa ni pamoja na vituo vya kulelea watoto.

11.5 Kukaribisha wamishionari kutoka nje ya Tanzania wenye Imani sawa na ya RAGT, na wenye nia ya kushirikiana na sisi katika kufanya kazi ya Mungu kwa mujibu wa Katiba hii.

11.6 Kutafuta wafadhili ndani na nje ya Tanzania kwa ajili ya kuisaidia RAGT kujiendeleza pasipo masharti yoyote yanayoweza kuathiri vibaya Imani ya RAGT.

Misingi ya Imani 12. RAGT inaamini kwamba;

12.1 **Biblia Takatifu.**

Biblia ni Neno la Mungu lililovuviwa na Roho Mtakatifu, na Yesu Kristo ni Mwokozi.

12.2 **Injili ya Yesu Kristo.**

Injili ni Habari Njema inayoleta wokovu na imewekwa wazi kwa kafara ya damu ya Yesu iliyomwagika Kalvari na wakati uliokubalika na Bwana kwa wokovu ni sasa.

12.3 **Wokovu.**

Kila atakayemwamini Yesu Kristo kuwa Bwana na Mwokozi wa Maisha yake binafsi na kuacha maovu sawa na Biblia inavyoeleza ataokoka, kwakuwa Wokovu ni katika Jina la Yesu pekee.

12.4 Ubatizo wa Maji mengi.

Kila aliyeokoka ni lazima abatizwe kwa ubatizo wa maji mengi yaani ubatizo ule wa Yesu Kristo (*Mt 3:15, Yoh 3:22-23*).

12.5 Ujazo wa Roho Mtakatifu na Kunena kwa lugha mpya.

Kila aliyeamini ni lazima apokee ahadi ya baba yaani ajazwe Roho Mtakatifu (*Mdo 2:1-4*).

12.6 Ishara na Miujiza.

Kila aliyeokoka, ishara na miujiza ya Yesu Kristo itafuatana naye.

- | | |
|-------------|--|
| Ushirikiano | RAGT itafanya kazi kwa kushirikiana na madhehebu yote yenye Imani ya kipentekoste yaliyo ndani na nje ya Tanzania. |
| Mwongozo | Kutakuwa na Mwongozo utakao jumuisha Taratibu na Kanuni mbalimbali zitakazo iongoza RAGT katika Utekelezaji wa majukumu yake ya kila siku. |

SURA YA NNE

UONGOZI

Uhiari wa
Uongozi

13. Uongozi/Utumishi na Utendaji katika RAGT ni wa hiari, na utazingatia Neno la Mungu (*Biblia Takatifu*) sawa na Imani yetu.

Nafasi ya
Uongozi

14. Nafasi ya juu ya uongozi ni ya Mungu. Hivyo viongozi wengine wote watapokea uongozi kutoka kwa Mungu.

Kamati Kuu

15. Wajumbe wa Kamati Kuu watakuwa ni;

15.1 Askofu Mkuu

15.2 Makamu Askofu Mkuu

15.3 Katibu Mkuu

15.4 Makamu Katibu Mkuu

15.5 Mhazini Mkuu

15.6 Afisa Utawala

Halmashauri
Kuu

16. Wajumbe wa Halmashauri Kuu watakuwa ni;

16.1 Kamati Kuu

16.2 Bodi ya Wadhamini

16.3 Maaskofu wa Kanda

16.4 Sekretarieti ya Halmashauri Kuu

16.5 Wenyeviti wa Idara na Kurugenzi zote
Kitaifa

16.6 Mwanasheria wa RAGT

Sekretarieti ya
Halmashauri
Kuu

17. Wajumbe wa Sekretarieti ya Halmashauri Kuu
watakuwa ni;

17.1 Katibu Mkuu

17.2 Makamu Katibu Mkuu

17.3 Afisa Utawala

17.4 Afisa Fedha

17.5 Mwanasheria wa RAGT

17.6 Makatibu Wakuu wa Kanda

17.7 Makatibu Wakuu wa Kurugenzi zote
Kitaifa

17.8 Makatibu Wakuu wa Idara zote Kitaifa

Kamati ya
Maadili

18. Wajumbe wa Kamati ya Maadili Kitaifa
watakuwa ni;

18.1 Makamu Askofu Mkuu

18.2 Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini RAGT

18.3 Mwanasheria wa RAGT

18.4 Askofu wa Kanda 1 atakayeteuliwa na
Kamati Kuu

Kanda

19. Kutakuwa na Kanda mbalimbali
zitakazoongozwa na Maaskofu wa Kanda. Kanda hizi
zitaundwa kwa msingi wa urahisi wa njia za usafiri ili
kuleta ufanisi wa Kiutendaji, na zitajumuisha Mkoa
zaidi ya Mmoja.

Maofisa wa
Kanda

20. Kanda itakuwa na viongozi wakuu wafuatao;

20.1 Askofu wa Kanda

20.2 Makamu Askofu wa Kanda

20.3 Katibu wa Kanda

20.4 Katibu Msaidizi wa Kanda

20.5 Mhazini/Mhasibu wa Kanda

Jimbo 21. Kutakuwa na Majimbo mbalimbali yatakayoongozwa na Maaskofu wa Majimbo. Kila Mkoa mmoja wa Utawala wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itakuwa ni Jimbo moja la RAGT.

Maofisa wa Jimbo 22. Jimbo litakuwa na viongozi wakuu wafuatao;

22.1 Askofu wa Jimbo

22.2 Makamu Askofu wa Jimbo

22.3 Katibu wa Jimbo

22.4 Katibu Msaidizi wa Jimbo

22.5 Mhazini/Mhasibu wa Jimbo

Wilaya 23. Kutakuwa na Wilaya zitakazoongozwa na Waangalizi wa Wilaya. Kila wilaya moja ya Utawala wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itakuwa ni Wilaya moja ya RAGT.

Maofisa wa Wilaya 24. Wilaya itakuwa na viongozi wakuu wafuatao;

24.1 Mwangalizi wa Wilaya

24.2 Mwangalizi Msaidizi wa Wilaya

24.3 Katibu wa Wilaya

24.4 Katibu Msaidizi wa Wilaya

24.5 Mhazini/Mhasibu wa Wilaya

Sifa za Uongozi 25. Kila kiongozi ndani ya RAGT atapaswa kuwa na sifa zifuatazo;

25.1 Kuwa kielelezo na mfano kwa tabia na mwenendo wa Kristo katika maisha yake ili watu wamwonapo wamtukuze Mungu.

25.2 Kuwa wakili mwaminifu wa mali ya Mungu, siri za Mungu na utauwa.

25.3 Kuwa Mjumbe wa habari njema za Yesu Kristo.

25.4 Awe anayefahamu uongozi wa Roho Mtakatifu, Kumkubali, Kumtii na mwenye kujua kujipambanua nafsi yake mwenyewe.

25.5 Awe tayari kutumia mali zake mwenyewe kwa ajili ya Injili.

25.6 Awe mwenye nia ya kuhimiza umoja wa Imani.

25.7 Awe ameokoka na kushuhudiwa kuwa ameokoka.

25.8 Awe amebatizwa ubatizo wa Maji mengi.

25.9 Awe mshirika mwaminifu aliyedumu kanisani kwa kipindi kisichopungua Mwaka mmoja.

Sifa za Askofu
Mkuu

26. Askofu Mkuu atapaswa kuwa na Sifa zifuatazo;

26.1 Awe ni Mchungaji anayetoka kwenye kanisa la RAGT lenye ustawi na maendeleo mazuri.

26.2 Awe mwenye sifa zilizotajwa katika Biblia (1Tim 3:1-7).

26.3 Awe Mchungaji Msimikwa wa RAGT kwa kipindi kisichopungua Miaka 10.

26.4 Awe amewahi kuwa Ofisa wa Kanda au Jimbo na kufanya vizuri kwenye uongozi wake.

26.5 Awe na elimu ya Theolojia angalau kwa Ngazi ya Shahada ya Kwanza kutoka katika Chuo kinachotambulika na RAGT.

26.6 Awe na Umri wa kuanzia Miaka 45.

Majukumu ya
Askofu Mkuu

27. Askofu Mkuu atakuwa na majukumu yafuatayo;

27.1 Atakuwa ndiye Mwenyekiti wa Vikao vya Kamati Kuu, Halmashauri Kuu pamoja na Mikutano Mikuu yote.

27.2 Atakuwa Mwakilishi na Msemaji Mkuu wa RAGT mahali popote ndani na nje ya Nchi.

27.3 Atatia saini kwenye vyeti vya Wachungaji wasimikwa.

27.4 Atahakikisha kuwa RAGT inaongozwa kwa misingi ya Katiba ya RAGT na Neno la Mungu.

27.5 Atawajibika kwa Halmashauri kuu na Mkutano Mkuu.

27.6 Atawajibishwa na Bodi ya Wadhamini kwa shauri linalohusu ubadhilifu wa Mali za RAGT.

27.7 Atakuwa ni mmoja wa watia saini kwenye akaunti za benki za Mfuko Mkuu.

27.8 Kutoa Maono na Mwelekeo wa Kanisa la RAGT.

Sifa za Makamu
Askofu Mkuu

28. Makamu Askofu Mkuu atakuwa na sifa zifuatazo;

28.1 Atapaswa kuwa na sifa zote za nafasi ya Askofu Mkuu.

Majukumu ya Makamu Askofu Mkuu 29. Makamu Askofu Mkuu atakuwa na majukumu yafuatayo;

29.1 Atakaimu nafasi ya Askofu Mkuu wakati Askofu Mkuu hayupo.

29.2 Atatekeleza majukumu yote atakayopangiwa na Askofu Mkuu.

29.3 Atakuwa Mshauri Mkuu wa Askofu Mkuu kwa Maswala yote yahusuyo maongozi ya RAGT.

29.4 Atakuwa ni mmoja wa watia saini kwenye Akaunti za benki za Mfuko Mkuu.

29.5 Atakuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili Taifa.

29.6 Atakuwa Mlezi Mkuu wa Idara zote.

29.7 Atawajibika kwa Askofu Mkuu na Halmashauri Kuu.

Sifa za Katibu Mkuu 30. Katibu Mkuu atapaswa kuwa na sifa zifuatazo;

30.1 Awe ni Mchungaji anayetoka kwenye kanisa la RAGT lenye ustawi na maendeleo mazuri.

30.2 Awe Mchungaji Msimikwa wa RAGT kwa kipindi kisichopungua Miaka 5.

30.3 Awe ameoau ameolewa, na mwenye Ndoa yenye ushuhuda mzuri.

30.4 Awe na elimu ya Theolojia angalau kwa Ngazi ya Diploma kutoka katika Chuo kinachotambulika na RAGT.

30.5 Awe na umri kuanzia Miaka 35.

30.6 Awe amewahi kuwa Ofisa wa Kanda au Jimbo na kufanya vizuri kwenye uongozi wake.

Majukumu ya
Katibu Mkuu

31. Katibu Mkuu atakuwa na majukumu yafuatayo;

31.1 Ndiye Mtendaji Mkuu wa shughuli zote za RAGT.

31.2 Atakuwa Msimamizi Mkuu wa nidhamu na Itifaki.

31.3 Atatoa taarifa ya Utendaji kazi wa RAGT katika Vikao vya Kamati Kuu, Halmashauri Kuu na Mkutano Mkuu.

31.4 Atatia saina kwenye vyeti vya Wachungaji wasimikwa.

31.5 Atakuwa ni mmoja wa watia saini kwenye Akaunti za benki za Mfuko Mkuu.

31.6 Atatunza kumbukumbu mbalimbali za Ofisi ya Makao Makuu, ikiwepo Mihutasari ya Vikao na nyaraka mbalimbali isipokuwa Mihuri ya Wadhamini.

31.7 Atakuwa Katibu wa Vikao vyote vya Kamati Kuu, Halmashauri Kuu na Mkutano Mkuu.

31.8 Atakuwa mwenyekiti wa Vikao vyote vya Sekretarieti ya Halmashauri Kuu.

31.9 Atatekeleza majukumu yote atakayopangiwa na Askofu Mkuu.

31.10 Ataweka saini katika Vitambulisho vyote vya watumishi wa RAGT.

31.11 Atawajibika kwa Askofu Mkuu na Halmashauri Kuu.

Sifa za
Makamu
Katibu Mkuu

32. Makamu Katibu Mkuu atakuwa na sifa zifuatazo;

32.1 Atapaswa kuwa na sifa zote za nafasi ya Katibu Mkuu.

Majukumu ya Makamu Katibu Mkuu 33. Makamu Katibu Mkuu atakuwa na majukumu yafuatayo;

33.1 Atakaimu nafasi ya Katibu Mkuu wakati Katibu Mkuu hayupo.

33.2 Atatekeleza majukumu yote atakayopangiwa na Katibu Mkuu.

33.3 Atakuwa Mshauri wa Katibu Mkuu kwa Maswala yote yahusuyo utendaji ndani ya RAGT.

33.4 Kusaidiana na Katibu Mkuu katika maswala yote ya ajira ndani ya RAGT.

33.5 Atakuwa Makamu Mwenyekiti katika vikao vyote vya sekretarieti ya Halmashauri Kuu.

33.6 Atafuatilia ustawi wa Idara zote Kitaifa na kuwasilisha taarifa ya Idara hizo katika Vikao vya Kamati Kuu na Halmashauri Kuu.

33.7 Atawajibika kwa Katibu Mkuu.

Sifa za Mhasibu/Mhazini Mkuu 34. Mhasibu/Mhazini Mkuu atapaswa kuwa na sifa zifuatazo;

34.1 Sifa zote za nafasi ya Katibu Mkuu.

34.2 Elimu ya Uhasibu/Fedha itakuwa ni sifa ya ziada.

34.3 Awe na umri kuanzia Miaka 35.

Majukumu ya Mhasibu/
Mhazini Mkuu 35. Mhasibu/Mhazini Mkuu atakuwa na Majukumu yafuatayo;

35.1 Atatunza kumbukumbu na taarifa zote za fedha na kuhakikisha kuwa taarifa hizo ni sahihi.

35.2 Ataandaa taarifa ya fedha ya Mapato na Matumizi kwa kushirikiana na Afisa Fedha, na kuiwasilisha kwenye Vikao vya Kamati Kuu, Halmashauri Kuu na Mkutano Mkuu.

35.3 Atakuwa Mshauri wa Askofu Mkuu kwa Maswala yahasuyo fedha.

35.4 Atakuwa ni mmoja wa watia saini kwenye Akaunti za benki za Mfuko Mkuu.

35.5 Atawajibika kwa Askofu Mkuu na Halmashauri Kuu.

35.6 Atahakikisha kuwa stakabadhi inatolewa kwa fedha yoyote inayopokelewa na kutunza kumbukumbu zake.

35.7 Atatumia fedha ya Mfuko Mkuu wa RAGT kwa mujibu wa bajeti iliyopitishwa na Kamati Kuu.

Sifa za Afisa
Utawala na
Afisa Fedha

36. Maafisa hawa wataajiriwa na RAGT kulingana na Taaluma zao. Sifa zao zitaainishwa kwenye Tangazo la Ajira husika.

Majukumu ya
Afisa Utawala

37. Afisa Utawala atakuwa na Majukumu yafuatayo:

37.1 Atafanya kazi zote atakazoagizwa kufanya na Katibu Mkuu na Makamu Katibu Mkuu.

37.2 Atakuwa Katibu wa Vikao vyote vya sekretarieti ya Halmashauri Kuu.

37.3 Kusimamia, Kushauri na Kuelekeza viongozi wa Idara zote katika Maswala mbalimbali ya Uongozi na Itifaki.

37.4 Atawajibika kwa Katibu Mkuu na Makamu Katibu Mkuu.

Majukumu ya
Afisa Fedha

38. Afisa Fedha atakuwa na Majukumu yafuatayo;

38.1 Atafanya kazi zote atakazoagizwa na Mhazini Mkuu.

38.2 Atashirikiana na Mhazini Mkuu katika kumshauri Askofu Mkuu juu ya maswala yote yahusuyo fedha.

38.3 Atakuwa ndiye Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa ndani wa fedha zote za RAGT kuanzia Ngazi ya Taifa mpaka Kanisa la mahali pamoja.

38.4 Ataandaa miongozo mbalimbali ya fedha na manunuzi ndani ya RAGT na kuleta mapendekezo hayo kwa Halmashauri Kuu.

38.5 Atatoa Elimu na ushauri juu ya Utunzaji wa kumbukumbu za Fedha.

38.6 Ataishauri Bodi ya Wadhamini juu ya Vyanzo mbalimbali vya mapato na Uanzishwaji wa Miradi mbalimbali.

38.7 Atawajibika kwa Mhazini Mkuu.

Mwanasheria
wa RAGT

39. Atakuwepo Mwanasheria wa RAGT atakayekuwa na Majukumu yafuatayo;

39.1 Atakuwa Mshauri Mkuu wa Askofu Mkuu juu ya Maswala yote ya kisheria yahasuyo RAGT.

39.2 Atasimamia kesi mbalimbali zilizo chini ya Bodi ya Wadhamini wa RAGT.

39.3 Ataishauri Bodi ya Wadhamini wa RAGT juu ya namna bora ya utunzaji wa mali za RAGT kisheria.

39.4 Ataandaa Mikataba mbalimbali ya kisheria ndani na nje ya RAGT.

39.5 Atathibitisha uhalali wa nyaraka mbalimbali za RAGT kwa nafasi ya KAMISHNA WA VIAPO.

39.6 Atawajibika kwa Katibu Mkuu.

SURA YA TANO

MIKUTANO NA VIKAO

Aina za
Mikutano

40. Kutakuwa na Mikutano Ifuatayo;

40.1 Mikutano Mkuu wa Kawaida

40.2 Mikutano Mkuu wa Uchaguzi

40.3 Mikutano Mkuu wa Dharura

Mikutano
Mkuu wa
Kawaida

41. Kutakuwa na Mikutano Mkuu wa Kawaida utakaofanyika kila mwaka mara moja na taarifa itatolewa kwa wajumbe miezi mitatu (3) kabla ya Mikutano huo.

Wajumbe wa
Mikutano
Mkuu wa
Kawaida

42. Wajumbe wa Mikutano Mkuu wa kawaida watakuwa ni;

42.1 Kamati Kuu

42.2 Bodi ya Wadhamini

42.3 Halmashauri Kuu

42.4 Sekretarieti ya Halmashauri Kuu

42.5 Wachungaji, Wainjilisti, Walimu, Mitume na Manabii wa RAGT pamoja na wake/waume zao wenye huduma zinazotambulika na Halmashauri Kuu.

42.6 Viongozi wote wa Taifa wa Idara na Kurugenzi.

42.7 Wamishionari wote wa RAGT.

42.8 Mzee Kiongozi mmoja (1) wa Kanisa la Mahali pamoja.

Majukumu ya
Mkutano
Mkuu wa
Kawaida

43. Majukumu ya Mkutano Mkuu wa Kawaida yatakuwa ni;

43.1 Kupokea taarifa mbalimbali za Maendeleo ya RAGT kutoka Kamati Kuu na Halmashauri Kuu.

43.2 Kurekebisha na Kupitisha marekebisha ya Katiba.

43.3 Kupokea taarifa ya Utendaji kazi wa Bodi ya Wadhamini.

43.4 Kusimika Wachungaji na watumishi wengine wa RAGT, pamoja na kutoa vyeti kwa wasimikwa.

43.5 Kumwondoa Madarakani kiongozi yeyote endapo;

43.5.1 Mkutano Mkuu utakuwa hauna Imani na Kiongozi huyo juu ya Maongozi yake.

43.5.2 Ubadhilifu wa Mali za RAGT uliothibitika.

43.5.3 Kiongozi kushindwa kutimiza Majukumu yake Kikatiba.

43.5.4 Kiongozi kuwa chanzo cha migogoro ndani ya RAGT.

43.5.5 Kung'ang'ania Madaraka.

43.5.6 Utovu wa nidhamu uliothibitishwa na Kamati ya Maadili.

Mkutano
Mkuu wa
Uchaguzi

44. Kutakuwa na Mkutano Mkuu wa Uchaguzi utakaofanyika kila baada ya Miaka Mitano (5) na taarifa ya Mkutano huo itatolewa kwa Wajumbe miezi mitatu (3) kabla ya Mkutano huo.

Wajumbe wa
Mkutano
Mkuu wa
Uchaguzi

45. Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa uchaguzi watakuwa ni Wajumbe wale wale waliotajwa katika Sura hii, Ibara ya Arobaini na mbili (42), kuanzia 42.1 hadi 42.7.

- Majukumu ya Mkutano Mkuu wa Uchaguzi 46. Mkutano Mkuu wa Uchaguzi utakuwa na majukumu yafuatayo;
- 46.1 Kuchagua viongozi wa RAGT ngazi ya Taifa, yaani Kamati Kuu (Isipokuwa Afisa Utawala), Wajumbe wa Bodi ya Wadhamini na Viongozi wa Kurugenzi zote Kitaifa.
- 46.2 Kufanya marekebisho au mabadiliko ya Katiba ya RAGT pale itakapobidi kufanya hivyo.
- Mkutano Mkuu wa Dharura 47. Kutakuwa na Mkutano Mkuu wa Dharura utakaoitishwa wakati wowote kutakapokuwa na jambo la dharura la kushughulikia. Taarifa ya Mkutano huo itatolewa kwa wajumbe wakati wowote.
- Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Dharura 48. Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Dharura watakuwa ni Wajumbe wale wale waliotajwa katika Sura hii, Ibara ya Arobaini na mbili (42), kuanzia 42.1 hadi 42.7.
- Majukumu ya Mkutano Mkuu wa Dharura 49. Mkutano Mkuu wa dharura utakuwa na jukumu maalumu tu lililosababisha Mkutano huo kuitishwa linalohitaji utatuzi wa haraka.
- Akidi/Idadi ya Wajumbe kwa Mikutano Mikuu yote 50. Akidi/Idadi halali ya wajumbe wa kila Mkutano Mkuu itapaswa kuwa zaidi ya nusu (1/2) ya wajumbe wa Mkutano Mkuu.

Vikao 51. Kutakuwa na vikao vya aina nne (4) ambavyo ni;

51.1 Kamati Kuu

51.2 Halmashauri Kuu

51.3 Sekretarieti ya Halmashauri Kuu

51.4 Kamati ya Maadili

Majukumu ya Kamati Kuu 52. Kamati kuu itakuwa na Majukumu yafuatayo;

52.1 Itasimamia utekelezaji wa Majukumu yote ya RAGT.

52.2 Itatoa taarifa ya Utendaji kwa Halmashauri Kuu.

52.3 Itasimamia nidhamu na maendeleo ya Watumishi mbalimbali na Wachungaji wa RAGT.

52.4 Itakuwa na vikao viwili (2) vya kawaida kwa Mwaka. Inaweza kuwa na vikao vingine vya dharura kulingana na hali ya Utendaji.

52.5 Itadumu madarakani kwa kipindi cha Miaka mitano (5). Ukomo wa kuchaguliwa ni Mihula mitatu (3) ya Uongozi. Kiongozi akitimiza Mihula mitatu, hatachaguliwa tena kwa nafasi ile ile, anaweza kuchaguliwa kwa nafasi nyingine.

Majukumu ya
Halmashauri
Kuu

53. Halmashauri Kuu itakuwa na Majukumu
yafuatayo;

53.1 Kupokea taarifa ya Utendaji kazi kutoka
kwenye Sekretarieti.

53.2 Kupokea mapendekezo kutoka Kanda, kwa
Wachungaji wanaotakiwa kusimikwa.

53.3 Kupitisha majina ya Wachungaji waliokidhi
vigezo au wenye sifa za kusimikwa.

53.4 Kupitisha bajeti ya RAGT kwa Mwaka wa
fedha unaofuata.

53.5 Kupokea taarifa mbalimbali za Kanda na
Idara.

53.6 Itateua Kamati Maalumu kwa kazi
Maalumu kama itakavyoona inafaa.

53.7 Kupitisha Kanuni na Miongozo
mbalimbali ya RAGT.

53.8 Kuidhinisha ajira mbalimbali za Ofisi Kuu.

53.9 Itakuwa na Mamlaka ya Kugawa Wilaya,
Majimbo na Kanda zenye sifa ya kujitegemea.

53.10 Kupendekeza Majina ya Viongozi wa Kamati Kuu yatakayopigiwa kura na Mkutano Mkuu kwenye Mkutano Mkuu wa uchaguzi.

53.11 Kupendekeza Majina ya watu Wawili (2) yatakayopelekwa kwenye Mkutano Mkuu wa Idara, kwa ajili ya kupigiwa kura kwa Nafasi za uongozi katika Kamati Kuu za Idara Taifa kwenye Uchaguzi Mkuu wa Idara.

Majukumu ya Sekretarieti

54. Sekretarieti ya Halmashauri Kuu itakuwa na Majukumu yafuatayo;

54.1 Kusimamia na kutekeleza maazimio yote ya Kamati Kuu na Halmashauri Kuu.

54.2 Itaandaa vikao vyote vya Kamati Kuu, Halmashauri Kuu na Mkutano Mkuu.

54.3 Kuandaa taarifa za utendaji kazi na kuziwasilisha kwenye Halmashauri Kuu na Mkutano Mkuu.

54.4 Kuandaa Agenda za Vikao vya Halmashauri Kuu na Mkutano Mkuu na kuziwasilisha kwa Kamati Kuu.

54.5 Kuandaa Kalenda ya kanisa kwa Mwaka mzima.

54.6 Kujibu hoja mbalimbali za kiutendaji kwenye Vikao vya Halmashauri Kuu na Mkutano Mkuu.

54.7 Kuandaa bajeti ya RAGT ya Mwaka mzima.

Majukumu ya
Kamati ya
Maadili

55. Kamati ya Maadili itakuwa na Majukumu yafuatayo;

55.1 Itakuwa na Mamlaka ya kumuita na kumuhoji Kiongozi yeyote, wa ngazi yoyote ili kujibu shutuma za kimaadili zitakazokuwa zinamkabili.

55.2 Itatoa Mapendekezo ya adhabu kwa Mkutano Mkuu juu ya Kiongozi yeyote aliyekutwa na hatia juu ya kosa la kimaadili alilolifanya.

55.3 Itashughulikia utatuzi wa migogoro yote ya kimaadili ambayo haina Jinai ndani yake. Kwa makosa yote yanayohusu Mali na yenye Jinai ndani yake yatashughulikiwa na Bodi ya Wadhamini.

Dokezo

Kamati hii ni ya Rufaa Kitaifa. Hivyo migogoro yote itashughulikiwa kwenye ngazi husika ya Uongozi kabla shtaka hilo halijafikishwa kwenye Kamati ya Maadili.

SURA YA SITA

FEDHA NA MALI

- Mapato 56. Mapato ya RAGT yatatokana na;
- 56.1 Sadaka na Michango mbalimbali toka kwa Washirika wa RAGT.
- 56.2 Misaada kutoka kwa wafadhili na wahisani mbalimbali wa ndani na nje ya Tanzania.
- 56.3 Miradi mbalimbali itakayobuniwa na Uongozi wa RAGT.
- Mfuko Mkuu 57. Utakuwepo Mfuko wa RAGT utakaofahamika kama Mfuko Mkuu au Genaral Fund.
- Mapato ya Mfuko Mkuu 58. Vyanzo vya Mapato ya Mfuko Mkuu ni;
- 58.1 Zaka za Wajumbe wa Kamati Kuu na Afisa Fedha.
- 58.2 Zaka za Wajumbe wote wa Halmashauri Kuu isipokuwa Wajumbe wa Bodi ya Wadhamini.

58.3 Zaka za Makanisa ya Mahali pamoja ya RAGT.

58.4 Sadaka na Michango mbalimbali ya Wafadhili wa ndani ya RAGT (*washirika mbalimbali na Makanisa ya RAGT*) na nje ya RAGT.

58.5 Mapato kutoka kwenye Miradi mbalimbali iliyo chini ya RAGT.

Utunzaji wa
Mfuko Mkuu

59. Mfuko Mkuu utatunzwa kwa utaratibu ufuatao;

59.1 Fedha za mfuko huu zitatunzwa benki kwenye akaunti ya RAGT.

59.2 Watia saini kwenye akaunti hii watakuwa wanne yaani Askofu Mkuu, Makamu Askofu Mkuu, Katibu Mkuu na Mhazini Mkuu, na wawili kati yao wanaweza kusaini hati ya kutoa fedha benki na muamala kufanyika.

59.3 Mhazini Mkuu kwa kushirikiana na Afisa Fedha watawajibika kutunza kumbukumbu zote muhimu za fedha na stakabadhi za malipo mbalimbali

Matumizi ya
Mfuko Mkuu

60. Mfuko huu utakuwa na kazi ya;

60.1 Kuhudumia ofisi za Makao Makuu pamoja
na uendeshaji wa RAGT kwa ujumla.

60.2 Kutoa rambirambi au huduma/msaada kwa
Mtumishi yeyote wa RAGT pale itakapobidi.

60.3 Kugharamia safari za Kamati Kuu.

60.4 Kulipa posho za Wajumbe wa Kamati Kuu.

Mfuko wa
Elimu

61. Utakuwepo Mfuko wa Elimu wa RAGT
utakaotunza fedha kwa ajili ya kutoa elimu kwa
Watumishi wa RAGT.

Mapato ya
Mfuko wa
Elimu

62. Vyanzo vya Mapato ya Mfuko wa Elimu ni;

62.1 Asilimia 5 ya Sadaka za kanisa la Mahali
pamoja za kila jumapili.

62.2 Asilimia 5 ya Makusanyo ya Mfuko Mkuu
kila mwezi.

62.3 Sadaka na Michango mbalimbali ya
Wafadhili wa ndani ya RAGT (washirika
mbalimbali na Makanisa ya RAGT) na nje ya
RAGT.

Utunzaji wa
Mfuko wa
Elimu

63. Mfuko wa Elimu utatunzwa kwa Utaratibu ufuatao;

63.1 Fedha za mfuko huu zitatunzwa benki kwenye akaunti Maalumu ya Elimu.

63.2 Watia saini kwenye akaunti hii watakuwa wanne yaani Katibu Mkuu, Mkurugenzi wa Kurugenzi ya Elimu na Mafunzo, Katibu wa Kurugenzi ya Elimu na Mafunzo, na Mhazini wa Kurugenzi ya Elimu na Mafunzo, na wawili kati yao wanaweza kusaini hati ya kutoa fedha benki na muamala kufanyika.

63.3 Mhazini wa Kurugenzi ya Elimu na Mafunzo atawajibika kutunza kumbukumbu zote muhimu za fedha na stakabadhi za malipo mbalimbali za mfuko huu.

Matumizi ya
Mfuko wa
Elimu

64. Mfuko huu utakuwa na kazi ya;

64.1 Kugharamia sehemu ya Ada na gharama zingine za wanafunzi wa Vyuo vya Biblia vilivyo chini ya RAGT.

64.2 Kulipa gharama za uendeshaji wa Vyuo vya Biblia vya RAGT na shule zote zilizo chini ya RAGT, isipokuwa vyuo au shule zilizo chini ya Kanda, Jimbo, Wilaya na Kanisa la Mahali pamoja.

64.3 Kulipa gharama za semina mbalimbali
zitakazoandaliwa kitaifa au kikanda chini ya
Uratibu wa Kurugenzi ya Elimu na Mafunzo.

Mfuko wa
Kanisa la
Mahali
pamoja

65. Utakuwepo Mfuko wa Kanisa la Mahali pamoja
utakaotumika kutunza fedha zote za Kanisa la
Mahali pamoja.

Mapato ya
Mfuko wa
Kanisa la
Mahali pamoja

66. Vyanzo vya Mapato ya Mfuko huu ni;

66.1 Sadaka za wakristo wote wanaofika
kuabudu kanisani.

66.2 Michango mbalimbali kwa ajili ya
kuendeleza kanisa na Idara zake.

66.3 Misaada kutoka kwa wafadhili mbalimbali
ndani na nje ya RAGT.

66.4 Mapato yatokanayo na miradi mbalimbali
iliyo chini ya kanisa la mahali pamoja.

Utunzaji wa
Mfuko wa
Kanisa la
Mahali
pamoja

67. Mfuko wa Kanisa la Mahali pamoja utatunzwa
kwa utaratibu ufuatao;

67.1 Fedha za mfuko huu zitatumizwa benki
kwenye akaunti ya Kanisa, isipokuwa kwa
makanisa yaliyo pembezoni mwa miji ambayo
hayajafikiwa na huduma za kibenki.

67.2 Fedha za sadaka zitahesabiwa na watu wasiopungua wawili, na taarifa ya sadaka hizo kujazwa kwenye kitabu maalumu cha Taarifa za fedha kisha waliohesabu watatia saini katika kitabu hicho baada ya kumaliza kujaza taarifa.

67.3 Watia saini katika akaunti ya benki watakuwa wanne ambao ni; Mchungaji Kiongozi, Katibu wa kanisa, Mhasibu wa Kanisa na Mzee mmoja wa Kanisa, na wawili kati yao wanaweza kusaini hati ya kutoa fedha benki na muamala kufanyika.

67.4 Mhasibu wa kanisa atawajibika kutunza kumbukumbu zote muhimu za fedha na stakabadhi za malipo mbalimbali za mfuko huu.

Matumizi ya
Mfuko wa
kanisa la
Mahali pamoja

68. Mfuko wa Kanisa la Mahali pamoja utakuwa na kazi ya;

68.1 Kulipa posho ya Mchungaji kutoka kwenye sadaka za Zaka, Shukrani, Malimbuko na Nadhiri. Sadaka hizi zitapaswa kwenda moja kwa moja kwa Mchungaji baada ya kuhesabiwa na kumbukumbu zake kutunzwa.

68.2 Kulipa gharama za safari za kihuduma za Mchungaji.

68.3 Kulipa kodi ya nyumba ya Mchungaji na gharama nyingine za nyumba ya Mchungaji.

68.4 Kulipa Zaka ya Sadaka Kuu/Dhabihu kwenye Mfuko Mkuu wa RAGT.

68.5 Kufanya maendeleo ya Kanisa.

68.6 Matumizi mengine ya Ofisi ya Mchungaji kama umeme, anwani ya posta, bili ya maji, nk.

68.7 Kulipa 5% ya Mfuko wa Elimu kutoka kwenye Sadaka Kuu/Dhabihu.

68.8 Kujenga nyumba binafsi ya Mchungaji.

Mifuko
mengine ya
RAGT

69. Kutakuwa na mifuko mingine ya fedha ndani ya RAGT kama;

69.1 Mfuko wa Kanda

69.2 Mfuko wa Jimbo

69.3 Mfuko wa Wilaya

69.4 Mifuko ya Idara za RAGT

Vyanzo vya
Mapato,
Utunzaji na
Matumizi

70. Vyanzo vya fedha vya Mfuko wa Kanda, Jimbo, Wilaya na Idara zote za RAGT, Utunzaji na matumizi yake, vimefafanuliwa kwa kina katika Mwongozo Mkuu wa RAGT.

Dokezo

Na ifahamike kwamba, yeyote atakayetoa mchango wake kwa ajili ya kuendeleza RAGT hatadai kurudishiwa wala hatadai upendeleo wa aina yoyote kwa RAGT. Alewe kwamba amemtolea Mungu.

SURA YA SABA

UCHAGUZI WA VIONGOZI

Uchaguzi wa
Viongozi wa
Kamati Kuu

71. Uchaguzi huu utakuwa ni wa kuchagua Askofu Mkuu, Makamu Askofu Mkuu, Katibu Mkuu, Makamu Katibu Mkuu na Mhazini Mkuu.

Usimamizi wa
Uchaguzi

72. Uchaguzi huu utasimamiwa na Wajumbe wa CPCT Taifa au uwakilishi wao. Unaweza pia kusimamiwa na viongozi wa Serikali ya eneo husika mahali ambapo uchaguzi utafanyika ikiwa kuna haja ya kufanya hivyo.

Utaratibu wa
Uchaguzi

73. Utaratibu ufuatao utatumika ili kupata Viongozi wa Kamati Kuu;

73.1 Halmashauri Kuu itapendekeza majina ya wanaofaa kuchaguliwa kwa nafasi ya Uongozi wa Kamati Kuu. Zoezi hili la kupendekeza majina litafanyika siku moja kabla ya Mkutano Mkuu wa Uchaguzi.

73.2 Kwa nafasi ya Askofu Mkuu, majina manne (4) yatapendekezwa, na kupelekwa kwenye Mkutano Mkuu ili kupigiwa kura na wajumbe wa Mkutano Mkuu kupata jina moja litakalopita kwa nafasi ya Askofu Mkuu.

73.3 Majina matatu (3) yaliyobaki baada ya kupatikana kwa Askofu Mkuu, yatapigiwa kura tena ili kumpata Makamu Askofu Mkuu.

73.4 Kwa nafasi ya Katibu Mkuu, Halmashauri Kuu itapendekeza Majina Manne (4) na kuyapeleka kwenye Mkutano Mkuu ili kupigiwa kura na wajumbe wa Mkutano Mkuu kupata jina moja litakalopita kwa nafasi ya Katibu Mkuu.

73.5 Majina matatu (3) yaliyobaki baada ya kupatikana kwa Katibu Mkuu, yatapigiwa kura tena ili kumpata Makamu Katibu Mkuu.

73.6 Kwa nafasi ya Mhazini/Mhasibu Mkuu, Halmashauri Kuu itapendekeza Majina Matatu (3) na kuyapeleka kwenye Mkutano Mkuu ili kupigiwa kura na wajumbe wa Mkutano Mkuu kupata jina moja litakalopita kwa nafasi ya Mhazini/Mhasibu Mkuu.

73.7 Washindi kwa nafasi zote hizo ni wale

watakaopata kura zaidi ya nusu (50%) ya kura za wajumbe wote wa Mkutano Mkuu.

73.8 Kwa nafasi zote za viongozi wanaochaguliwa, majina ya watu wanaopendekezwa yakishasomwa na Msimamizi wa uchaguzi, watu waliosomwa watatakiwa kusimama mbele ya Mkutano Mkuu na kusalimia kwa kujitambulisha. Hakutakuwa na nafasi ya kufanya kampeni ya namna yoyote kwani haya ni maongozi ya kiroho.

Makabidhiano
ya Uongozi

74. Viongozi wa Kamati Kuu waliopita watakabidhi uongozi kwa viongozi wapya wa Kamati Kuu katika muda usiozidi siku thelathini (30) tangu tarehe ya uchaguzi kupita.

74.1 Makabidhiano ya Uongozi yatafanyika katika ofisi za Makao Makuu ya RAGT.

Kuondolewa
Madarakani

75. Kiongozi ataondolewa Madarakani kwa sababu zifuatazo;

75.1 Akiwa ametenda dhambi na kuthibitika.

75.2 Akipata ugonjwa uliothibitishwa na madaktari wawili (2), utakaomfanya ashindwe kutimiza majukumu yake Kikatiba.

75.3 Akifariki dunia kabla ya Muhula wake wa

Uongozi kumalizika.

75.4 Kujiuzulu mwenyewe.

75.5 Utovu wa nidhamu.

75.6 Kutokuwepo mahali pake pa kazi kwa kipindi cha miezi mitatu (3) bila taarifa rasmi ya maandishi. Kwa walioajiriwa wao watafuata masharti ya Mikataba ya ajira zao.

Dokezo

Baada ya kiongozi yeyote kuondolewa Madarakani kwa sababu zilizotajwa hapo juu, Kanuni za Uchaguzi zitafuatwa ili kujaza nafasi iliyoachwa wazi. Nafasi ya kiongozi iliyo wazi itapaswa kujazwa ndani ya Miezi sita (6).

Uchaguzi wa
Kanda

76. Utaratibu ufuatao utatumika ili kupata Viongozi wa Kanda.

76.1 Wajumbe wa Mkutano wa kanda watapendekeza majina ya watu wanaofaa kuwa viongozi wa kanda.

76.2 Kwa kila nafasi, majina mawili (2) ya juu yatakapopata kura nyingi, yatapigiwa kura na wajumbe wa Mkutano wa Kanda ili kupata kiongozi wa nafasi husika.

76.3 Washindi kwa nafasi zote hizo ni wale watakaopata kura zaidi ya nusu (50%) ya kura za wajumbe wote waliohudhuria Mkutano wa Kanda.

76.4 Uchaguzi huu utasimamiwa na Wajumbe wa Kamati Kuu au Mwakilishi wa Kamati Kuu atayechaguliwa na Kamati Kuu kusimamia kazi hiyo. Ikiwa atakayechaguliwa kusimamia uchaguzi huo si mjumbe wa Kamati Kuu, basi Kamati Kuu itaandika barua kwa aliyechaguliwa kusimamia uchaguzi huo na nakala ya barua itapelekwa kwenye uongozi wa Kanda husika kwa taarifa.

76.5 Kwa nafasi zote za viongozi wanaochaguliwa, majina ya watu wanaopendekezwa yakishasomwa na Msimamizi wa uchaguzi, watu waliosomwa watatakiwa kusimama mbele ya Mkutano wa Kanda na kusalimia kwa kujitambulisha. Hakutakuwa na nafasi ya kufanya kampeni ya namna yoyote kwani haya ni maongozi ya kiroho.

76.6 Wajumbe wa Mkutano wa Kanda ni Wachungaji wote wa Kanda husika, na Viongozi wa Kanda wa Idara zote.

Uchaguzi wa
Jimbo na
Wilaya

77. Utaratibu ufuatao utatumika ili kupata Viongozi wa Jimbo na Wilaya;

77.1 Chaguzi hizi zitafuata mfumo wa Uchaguzi wa Kanda.

77.2 Uchaguzi wa Jimbo utasimamiwa na Viongozi wa Kanda.

77.3 Uchaguzi wa Wilaya utasimamiwa na Viongozi wa Jimbo.

77.4 Kama uongozi wa Jimbo haupo, basi Uongozi wa Kanda utasimamia Uchaguzi wa Wilaya.

Chaguzi za
Idara zote za
RAGT

78. Chaguzi za Viongozi wa Idara zote (Wanaume, Wanawake, Vijana, Watoto, Kwaya na Sifa, Injili, Umisheni na Maombi) zitafuata utaratibu ufuatao katika kupata Viongozi;

78.1 Chaguzi hizi zitasimamiwa na Viongozi wa juu wa ngazi husika ya Uchaguzi.

78.2 Kwa nafasi ya Viongozi wa Taifa wa Idara, Chaguzi hizo zitasimamiwa na wajumbe wa Kamati Kuu. Wanaweza kuwepo wajumbe wote au kutuma wawakilishi au mwakilishi.

Kanuni za
Jumla za
Uchaguzi

79. Kanuni zifuatazo zitatumika kwa Chaguzi zote ndani ya RAGT;

79.1 Viongozi katika nafasi zote za maongozi ndani ya RAGT watadumu madarakani kwa kipindi cha Miaka mitano (5).

79.2 Ukomo wa kuchaguliwa kwa kiongozi yeyote ni Mihula mitatu (3) ya Uongozi. Kiongozi akitimiza Mihula mitatu, hatachaguliwa tena kwa nafasi ile ile, anaweza kuchaguliwa kwa nafasi nyingine.

79.3 Kiongozi yeyote anaweza kuondolewa madarakani wakati wowote itakapoonekana kuna sababu ya kufanya hivyo kwa maslahi mapana ya RAGT.

79.4 Kiongozi ataondolewa madarakani kwa sababu zifuatazo;

79.4.1 Akiwa ametenda dhambi na kuthibitika.

79.4.2 Akipata ugonjwa uliothibitishwa na madaktari wawili (2), utakaomfanya ashindwe kutimiza majukumu yake kikatiba.

79.4.3 Akifariki dunia kabla ya muhula wake wa Uongozi kumalizika.

79.4.4 Kujiuzulu mwenyewe.

79.4.5 Utovu wa nidhamu.

79.4.6 Kutokuwepo mahali pake pa kazi kwa kipindi cha miezi mitatu (3) bila taarifa rasmi ya maandishi.

79.5 Kura zilizopigwa zitahesabiwa mahali pa wazi ndani ya ukumbi ambao uchaguzi husika unafanyika chini ya usimamizi wa kiongozi husika anayesimamia uchaguzi huo.

79.6 Kura zote zitapigwa kwa maandishi na zitakuwa ni kura za siri.

79.7 Mahali ambapo jina linalopendekezwa kwa nafasi husika litakuwa ni jina moja, basi kura ya wazi ya NDIYO au HAPANA itapigwa na wajumbe wa Mkutano husika.

79.8 Matokeo ya uchaguzi yatatolewa mara tu baada ya zoezi la kuhesabu kura kukamilika kwa kila ngazi husika.

79.9 Kiongozi yeyote anapaswa kuwa na nafasi moja tu ya Uongozi. Inapotokea anachaguliwa

kwa nafasi ya juu zaidi au nafasi nyingine yoyote, basi italazimu ajiuzulu kwenye nafasi yake ya uongozi wa awali. Kwa muktadha huu, zile huduma tano (5) yaani Uchungaji, Utume, Unabii, Uinjilisti na Ualimu hazihesabiwi kuwa ni nafasi za maongozi bali ni Utumishi.

79.10 Viongozi wa Kurugenzi zote watapendekezwa na kuchaguliwa kwenye Mkutano Mkuu wa uchaguzi. Mkutano Mkuu ndiyo utakaopendekeza majina na kuchagua.

79.11 Sifa za viongozi wa Idara zote zimeanishwa kwenye miongozo ya idara husika.

79.12 Kabla ya chaguzi kufanyika, wasimamizi wa uchaguzi kwa ngazi zote watapaswa kuhakiki uhalali wa wajumbe wa Mkutano huo wa Uchaguzi na kuhesabu idadi ya wajumbe wote halali.

79.13 Mahudhurio ya mkutano wa uchaguzi yatapaswa kuchukuliwa kwa maandishi na yawe yamesainiwa na wajumbe wote pamoja na kuonesha mahali wanakotoka na mawasiliano yao.

79.14 Kabla ya Uchaguzi kufanyika, viongozi waliopo madarakani italazimu wajiuzulu kwanza kabla ya zoezi la Uchaguzi wa viongozi wanya kufanyika.

SURA YA NANE

UTATUZI WA MIGOGORO

Uwasilishaji
wa Shauri

80. Mtumishi yoyote wa RAGT atakayekuwa na lalamiko, atawasilisha lalamiko lake kwa njia ya Maandishi katika ngazi husika ya Uongozi wake kabla shauri hilo halijapanda kwenda ngazi ya juu kimamlaka.

Taratibu za
Utatuji wa
Mgogoro

81. Kila mgogoro ndani ya RAGT utatatuliwa kwa njia ya mazungumzo na makubaliano kupitia vikao halali vya RAGT. Vikao hivyo ni;

81.1 Halmashauri ya Kanisa la Mahali pamoja.

81.2 Uongozi wa Wilaya

81.3 Uongozi wa Jimbo

81.4 Uongozi wa Kanda

81.5 Kamati Kuu

81.6 Halmashauri Kuu

81.7 Kamati ya Maadili

81.8 Mkutano Mkuu

Nafasi ya
Kusikilizwa

82. Kila mlalamikaji au mtuhumiwa atapewa nafasi ya kusikilizwa/kujitetea mbele ya kikao husika kabla kikao hicho hakijafanya maamuzi juu ya shauri lake. Maamuzi yote yatafanyika bila upendeleo kwa upande wowote.

Kukata Rufaa

83. Kwa shauri litakalokuwa limehitimishwa na Mkutano Mkuu, mlalamikaji/mlalamikiwa ana haki ya kukata rufaa kwenda CPCT, Ofisi ya Msajili wa Jumuiya za Kiraia na Mahakamani ikiwa ataona Mkutano Mkuu haujamtendea haki juu ya shauri lake.

SURA YA TISA

MABADILIKO YA KATIBA

Muda wa
Mabadiliko

84. Katiba hii inaweza kubadilishwa wakati wowote itakapoonekana kuna haja ya kufanya hivyo.

Mkutano
utakaofanya
Marekebisho

85. Mkutano Mkuu wa kawaida au Mkutano Mkuu wa Uchaguzi ndiyo wenye mamlaka ya kurekebisha na kupitisha mabadiliko ya Katiba hii.

Akidi/Idadi ya
Wajumbe

86. Idadi ya Wajumbe wa Mkutano Mkuu utakaofanya marekebisho ya Katiba na kuipitisha itapaswa kuwa $\frac{3}{4}$ (75%) au zaidi ya Wajumbe wote waliohudhuria Mkutano Mkuu husika.

SURA YA KUMI

BODI YA WADHAMINI

Uwepo wa
Bodi ya
Wadhamini

87. Itakuwepo Bodi ya Wadhamini wa RAGT iliyosajiliwa na Mamlaka ya Serikali kwa Jina la THE REGISTERED TRUSTEES OF REDEEMED ASSEMBLIES OF GOD TANZANIA.

Idadi ya
Wajumbe

88. Bodi ya Wadhamini itakuwa na wajumbe wasiopungua sita (6) na wasiozidi nane (8).

Sifa na
Majukumu ya
Bodi ya
Wadhamini

89. Sifa na Majukumu ya wajumbe wa Bodi ya Wadhamini yameainishwa katika Katiba ya Bodi ya Wadhamini ya RAGT.

SURA YA KUMI NA MOJA

IDARA NA KURUGENZI

Idara 90. Kutakuwa na Idara sita (6) ndani ya RAGT, ambazo ni;

90.1 Idara ya Wanaume.

90.2 Idara ya Wanawake (WWM).

90.3 Idara ya Vijana (VWM).

90.4 Idara ya Watoto.

90.5 Idara ya Kwaya na Sifa.

90.6 Idara ya Injili, Umisheni na Maombi.

Kurugenzi 91. Kutakuwa na Kurugenzi mbili (2) ndani ya RAGT, ambazo ni;

91.1 Kurugenzi ya Elimu na Mafunzo.

91.2 Kurugenzi ya Habari na Mawasiliano.

Dokezo

*Idara na Kurugenzi hizi zitaendeshwa sawa na
Miongozo na Kanuni zilizotungwa kusimamia Idara
na Kurugenzi hizo.*

SURA YA KUMI NA MBILI

KUVUNJIKWA KWA DHEHEBU

- | | |
|----------------------|--|
| Uhiari wa Kuvunjika | 92. Kwakuwa Redeemed Assemblies of God Tanzania ni Taasisi ya Kidini inayoendeshwa kwa misingi ya Neno la Mungu, sisi hatutarajii kuona Dhehebu likivunjika, isipokuwa kwasababu zilizo nje ya uwezo wetu au ikiwa ni takwa la serikali. |
| Mkutano utakaojadili | 93. Mkutano Mkuu wa Dharura ndiyo utakaojadili ajenda ya kuvunjika au kufutwa kwa Dhehebu. |
| Akidi/Idadi | 94. Akidi/Idadi ya Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Dharura utakaojadili ajenda ya kuvunjika au kufutwa kwa dhehebu itapaswa kuwa zaidi ya nusu (1/2) ya wajumbe wa Mkutano Mkuu. |
| Ugawaji wa Mali | 95. Bodi ya Wadhamini wa Redeemed Assemblies of God Tanzania ndiyo itakayokuwa na Mamlaka ya kugawa mali za dhehebu kwa kufuata uchangiaji wa kila kanisa la mahali pamoja na mshirika mmoja |

mmoja, ikiwa ni pamoja na kusimamia ulipaji wa madeni yote.

Dokezo

96. Kwakuwa RAGT haitarajii kuona dhehebu likivunjika, basi yule atakayeona ameshindwa kutimiza matakwa ya Katiba hii, kanuni na miongozo mbalimbali ya RAGT, basi itamlazimu kuondoka ndani ya Redeemed Assemblies of God Tanzania.

SURA YA KUMI NA TATU

MENGINEYO

- | | |
|------------------------|--|
| Uwepo wa Kanuni | 97. Kutakuwa na Kanuni mbalimbali zitakazotungwa na kupitishwa na Halmashauri Kuu ili kuwezesha utekelezaji mzuri wa Katiba hii. Kanuni hizi zitahesabika kuwa ni sehemu ya Sheria za RAGT. |
| Sensa | 98. Kutakuwa na Sensa ya Makanisa na washirika wote wa RAGT kila baada ya Kipindi cha Miaka Mitano (5). |
| Vyombo vya Mawasiliano | 99. RAGT itamiliki na kuendesha Vyombo mbalimbali vya Mawasiliano kama vile Radio, Televisheni, Gazeti, Majarida, Vitabu, Machapisho Mbalimbali, Tovuti, Barua pepe, Mitandao ya Kijamii, Anwani za Posta, nk. |
| Uhamisho | 100. RAGT inaamini katika WITO alioitiwa mtu juu ya eneo husika. Kwa kuzingatia hilo, hakutakuwa na uhamisho kwa Watumishi wasimamizi wa makanisa ya RAGT (Wachungaji), isipokuwa |

Mtumishi husika ametenda dhambi na kuthibitika,
au Mtumishi yeye mwenyewe kuomba kuhama/
kubadilishana kituo na Mtumishi mwingine wa
RAGT.

Kustaafu 101. Utumishi wa Kumtumikia Kristo hauna
kustaafu. Pamoja na hilo, ni ukweli ulio dhahiri
kuwa uzeeni miili ya wanadamu huchoka na
kupungukiwa nguvu. Mtumishi atakapofikia hatua
hiyo, RAGT itakuwa na utaratibu Maalumu wa
Utoaji wa Mafao kwa Watumishi wazee waliotumika
kwa Uaminifu ndani ya RAGT. Mpango huu wa
Utoaji Mafao kwa Watumishi wa aina hiyo
umefafanuliwa kwa kina katika Mwongozo wa
RAGT.

Bendera 102. RAGT itakuwa na bendera itakayotumika kwa
mtumizi mbalimbali ya kiofisi na kihuduma. Bendera
hiyo itakuwa ni ya kitambaa cheupe chenye nembo
ya RAGT katikati.

Kufutwa kwa
Katiba ya 1994 103. Katiba ya Redeemed Assemblies of God
Tanzania ya Mwaka 1994 iliyorekebishwa 1995
imefutwa rasmi.

Imepitishwa na Mkutano Mkuu wa:
Redeemed Assemblies of God Tanzania (RAGT)
Tarehe 4 Septemba 2024
Dodoma, Tanzania.